

)

TANGAZO LA SERIKALI Na. 321 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

AMRI

(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1))

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MGUSU YA MWAKA 2023

- | | |
|--|---|
| Jina | 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mgusu ya Mwaka 2023. |
| Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355 | 2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji. |
| Mpango wa jumla na kina wa eneo | 3. Mipango ya Jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Geita. |

—————
JEDWALI
—————

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 394603MS, 9684845KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa 149⁰ kwa umbali wa kilometa 2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira-nukta 395932MS, 9683352KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mpaka wa hifadhi ya msitu wa Geita upande wa Mashariki katika uelekeo wa 106⁰ kwa umbali wa kilometa 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 396388MS, 9683572KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa 110⁰ kwa umbali wa kilometa 1.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira-nukta 396213MS, 9685272KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa 124⁰ kwa umbali wa kilometa 0.24 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira- nukta 395119MS, 9685861KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa 104⁰ kwa umbali wa kilometa 0.87 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 394533MS, 9685215KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 127⁰ ukikutana na barabara ya Mgusu kwa umbali wa kilometa 0.37 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi*